Mungu Anamanisha Anachosema (God Means What He Says)

Na

Alex. S. Sadat

Mungu Anamanisha Anachosema

Na

Alex S. Sadat

Decemba 01, 2020

Mungu Anamanisha Anachokisema

Moja ya vitu tunavyo viona na kujifunza katika Biblia miongoni mwa nyingine ni kile alichokifanya Mungu kwenye miji ya Sodoma na Gomora. Tunamuona Ibrahimu ana bembeleza kwa ajili ya miji hii kwamba ikiwezekana Mungu aziache (Mwanzo 18:16-33). Lakini kwa sababu hawakubadilika kutoka katika uovu wao, Mungu akaona ni vyema aihangamize miji hii. Katika (ms. 23-25) tunamwona Ibrahimu anaongea na Mungu ana muuliza kama akipata watu hamsini wenye haki waaminifu katika mji, Mungu akasemaa hataiangamiza miji; hakika, Ibrahimu alitaka kujua kama Mungu angewafagia watu wote kwenye miji ile pamoja wenye haki. Lakini Mungu hakumuua Lutu na familia yake. Tunajifunza mengi kwenye somo hili lakini zaidi ya yote ni huruma ambayo Ibrahimu alikuwa nayo juu ya watu wa Sodoma na Gomora, angeweza kumwomba Mungu akamuacha mpwa wake Lutu lakini huo ungekuwa ni unafiki. Hiyo haikumbadilisha Mungu mawazo kwa sababu watu walioishi kwenye miji hiyo miwili walikuwa zaidi ya waovu. Tunaweza kuwa werevu tuwezavyo lakini linapokuja swala au mambo fulani, Mungu hubadilisha kila kitu na ndivyo ilivyo kuwa kwa watu wa Sodoma na Gomora. Walidhani ni werevu kuliko muumba.

Alipo muumba mwanadamu na kumweka katika bustani, alitarajia kiumbe kutii maagizo yote walioambiwa. Waliambiwa wasile matunda ya mti wa mema na mabaya la sivyo wangekufa (Mwa.2:15-17). Na kwa sababu walifanya dhambi, hakukuwa na njia nyingine ya kuwaokoa kwa sababu tayari walishaonywa. Walitakiwa kufuata maagizo ambayo walipewa; kama ilivyo leo Yesu ameweka hatua za wokovu ili kwamba tuweze kufuata, lakini mwanadamu ameamua kutofuata na kutofanya kilichoamuliwa kufanya, badala yake tunafanyya yale tuliokatazwa kufanya. Na unajua tunaposhindwa kufanya alichotuagiza Mungu nini kinatokea? Tunakufa. Ni nini sababu ya kifo cha kiroho kwa Mkristo? Dhambi. 1 Kor. 15:56, "*Ungu wa mauti ni dhambi, nguvu za dhambi ni torati.*" Tukifanya dhambi tunakufa na Mungu amekwisha tuambia na kutuonya kabla kwamba ye yote anayefanya mambo haya atakufa, anamanisha asemacho. Alipoweka hatua za wokovu kwa mwanadamu alimanisha kwamba tuzifuate hatua hizo. Katika Yakobo 1:15, "*Halafu ile dhaambi ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti.*" (KJV). "*Mtu akimwona ndugu yake anatenda dhambi isiyo ya mauti, ataomba, na Mungu atampa uzima kwa ajili ya hao watendao dhambi isiyo ya mauti. Iko dhambi iliyo ya mauti. Sisemi ya kwamba ataomba kwa ajili ya hiyo.*" (1 Yoh. 5:16).

Wapo watu wengi tunaowasoma kwenye maandiko ambao hawakumtii Mungu na waliwekwa katika adhabu kwa ajili ya makosa yao. Hebu tuone ni jinsi gani Mungu aliwaadhibu walipokosa, nah ii inajumuisha na sisi leo hii kwamba tusipofanya kile alichotuagiza kufanya:

Kaini na Abili, walimtolea Bwana dhabihu na akaikubali ya Abili na kukataa ya Kaini (Mwa.4:4-5). Tayari Mungu alikuwa ameshawaambia cha kuleta na kwa imani

Heb. 11:4, Kaini hakufanya kama walivyoambiwa na alifukuzwa kutoka machoni pa Mungu (Mwa.4:14-15). Ayubu 15:20-24; Zab. 51:11; Hes. 35:19-21. Na unajua nini kinachotokea Mungu anapokufukuza kutoka machoni pake? Unakufa!

Mwanadamu akawa mwovu sana na Mungu akasema ataangamiza viumbe hai vyote (Mwa.6:5-6). Alisubiri kwa miaka 120 wakati Nuhu alipoiandaa Safina alafu Mungu akaleta gharika (Mwa. 6:3; 1 Pet. 3:20).

Yesu alisema, "*mkumbuke mke wa Lutu*" (Luka 17:32). Aliambiwa asiangalie nyuma wakati yeye na familia yake walipokuwa wakitoka katika miji ya Sodoma na Gomora, lakini alitazama nyuma na akawa nguzo ya chumvi (Mwa. 19:26). Mungu humanisha asemalo kama sivyo angeweza kumwokoa mke wa Lutu, ndivyo ilivyo kwetu leo.

Mungu alimwambia Musa, "*nena na mwamba*" ili utoe maji kwa ajili ya wana wa Israeli (Hes. 20:8-11). Lakini Musa aliupiga mwamba mara mbili kwa fimbo yake. Na kwa sababu ya kosa hili aliruhusiwa kuona nchi ya ahadi, lakini hakuruhusiwa kuingia (Hes. 20:12; Kumb34:1-4). Mungu anamanisha asemalo na sote tunapaswa kufuata alichokiagiza.

Mungu alimwambia Haruni na watoto wake watumie moto wa kwenye madhabahu kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa (Law.6:9), lakini Nadabu na Hahu walileta moto wa kigeni kutoka kwenye vyanzo vingine na Mungu aaliwaua wote (Law. 10:1-2). Namkumbuka Ellis kwenye somo hili alipofundisha kule Shirati kwenye mkutano uliojumuisha makanisa yote ya wilaya ile.

Mungu alichagua kabila la Lawi ili kubeba sanduku la Mungu na mtu yeyote hakuruhusiwa kugusa, la sivyo wangekufa (Hes. 4:15). Katika tukio moja sanduku lilibebwa kwenye mkokoteni mpya na Uza akanyoosha mkono wake ili kushika sanduku lisianguke wakati wanyama walipokuwa wakijikwa; Mungu alimwua palepale. Wakati mwingine mwanadamu hujiona kuwa na akili kuliko Mungu lakini mwisho wake ni shida tupu.

Mfalme Sauli aliagizwa kuwaua Waamaleki na vyote walivyokuwa navyo (Isa.15:3). Lakini Sauli alimwacha Agagi na "*vyote vilivyokuwa vizuri*" na kila kitu (Isa. 15:9). Hatakama Sauli alianza kuwalaumu watu, Mungu alimnyang'anya ufalme.

Sasa vipi kuhusu sisi leo hii? Je Mungu anauhakika na asemacho kuhusu "MBINGU" tukifanya maakosa anasema kwamba "JEHANAMU" inatusubiri.?

"*Mtafuteni BWANA maadaamu anapatikana, mwiteni maadamu yu karibu; mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki aache mawazo yake; na amrudie BWANA naye atamrehemu na arejee kwa Mungu wetu naye atamsamehe kabisa.*" (Isa. 55:6-7). Nakumbuka Ellis alivyokuwa akielezea kuhusu Sanduku la Agano na Uza.

Ndugu, mara zote Mungu humanisha asemacho.